

copy

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA UJENZI

Mkatoba huu umesainiwa leo tarehe 23 mwezi 10 2021

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VETA KAGERA, S.L.P. 906, BUKOBWA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkatoba huu atajulikana kama Mwajiri) kwa upande mmoja;

NA

JOHANNES BONIEIRSE NDYKEZI S.L.P. 0754507683 MWANZA (ambaye katika Mkatoba huu atajulikana kama Fundi) kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya KWIMBA;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya KWIMBA;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya KUPIGA (LIPU) RIPU NJE NA NDANI ZA KIBANDA CHA MWANZI

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo wa vifaa vya Ujenzi (Schedule of materials) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 280,000/=, Fundi atafanya kazi ya KUPIGA RIPU kwa masharti yaliyo katika Mkatoba huu. Katika Mkatoba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama Gharama ya Ufundi

2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (*CONTRACT SUM ADJUSTMENT*)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundi;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi;na
- (f) Baada ya kukamilika kwa Muda wa matazamio :5% ya Gharama ya Ufundi.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUHIRISHA KAZI

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 23 mwezi 10 2021 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.
- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 21 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.
- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

- (a) ^{KUJENGA} Kujenga RIPY na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;
- (b) Kumpatia Mwajiri ratiba ya kazi (*work programme*) ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kusaini Mkataba huu ili kupata kibali cha Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA

Jina: JULIANA KUMARA Saini: [Signature]

Wadhifa: KAIMU KAIMU MKUU Tarehe: 23/10/2021

Mbele ya (Shahidi)

V.T.C PRINCIPAL
VOCATIONAL TRAINING CENTRE
KAGERA
BOX 906, BUKOBA

Jina: JOHANA AZZA Saini: [Signature]

Wadhifa: MWANASIS Tarehe: 23/10/2021

IMESAINIWA NA FUNDI

Mbele ya

Jina: JOHANNES BONIFASI NDUKESI Saini: [Signature]

Wadhifa: FUNDI MKUU Tarehe: 23/10/2021

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ALISTIDES CHARLES JIM Saini: A. Charles

Wadhifa: Fundi msaidizi Tarehe: 23/10/2021